

Swahili B – Higher level – Paper 2
Swahili B – Niveau supérieur – Épreuve 2
Swahili B – Nivel superior – Prueba 2

Tuesday 7 November 2017 (morning)

Mardi 7 novembre 2017 (matin)

Martes 7 de noviembre de 2017 (mañana)

1 h 30 m

Instructions to candidates

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Section A: choose one task. Each task is worth **[25 marks]**.
- Section B: write a personal response to the stimulus provided. The task is worth **[20 marks]**.
- The maximum mark for this examination paper is **[45 marks]**.

Instructions destinées aux candidats

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Section A : choisissez une tâche. Chaque tâche vaut **[25 points]**.
- Section B : exprimez votre opinion personnelle sur la réflexion fournie. La tâche vaut **[20 points]**.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est de **[45 points]**.

Instrucciones para los alumnos

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Sección A: elija una tarea. Cada tarea vale **[25 puntos]**.
- Sección B: escriba una opinión personal al estímulo provisto. La tarea vale **[20 puntos]**.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es **[45 puntos]**.

Sehemu A

Kamilisha **mojawapo** wa kazi zifuatazo. Andika maneno 250 hadi 400.

1. Utofauti wa tamaduni

Unaishi katika nchi inayozungumzwa Kiswahili na mji wako umewavutia wahamiaji wengi wageni, suala ambalo limesababisha utofauti wa tamaduni. Andika katika blogu ambapo utajadili faida na changamoto za utofauti wa tamaduni katika jamii.

2. Mila na desturi

Unaishi katika nchi inayozungumzwa Kiswahili kwa mara ya kwanza ambapo familia moja imekukaribisha uishi nayo na baadhi ya mila na desturi ni ngeni kwako. Jana, uliaibika kwa sababu ulikosa kufuata jambo moja la kitamaduni katika nchi hiyo bila kukusudia. Andika kwenye shajara ukieleza kilichotokea, na kile ulichosoma kutokana na tukio hilo.

3. Afya

Marafiki zako wengi wamefanya maamuzi fulani ya chakula (kama vile kuepuka nyama, maziwa na mafuta). Uliwahoji wawili wao kuhusu sababu za uamuzi wao. Andika mahojiano hayo, yatakayochapishwa katika sehemu ya 'Afya' ya jarida la shule yako.

4. Burudani

Pesa ina jukumu muhimu katika michezo siku hizi. Umeombwa utoe hotuba kwa wanafunzi wenzako kuhusu upande chanya wa hali hii. Andika hotuba yako.

5. Sayansi na teknolojia

Kampuni nyingi za usafiri wa umma zinaanza kuwapa wasafiri wao huduma za bure za Wi-Fi. Hata hivyo, kampuni ya mabasi katika eneo unaloishi bado haina huduma hii. Andika barua kwa mkurugenzi wa kampuni hiyo ukieleza umuhimu na faida ambazo huduma ya bure ya intaneti inaweza kuwa nazo kwa kampuni hiyo.

Sehemu B

Kulingana na kichocheo kifuatacho, toa jibu lako binafsi na ulithibitisha. Chagua maandiko yoyote uliyoyasoma darasani. Andika maneno kati ya 150 na 250.

6. Katika dunia yetu, vijana wanastahili kujifunza lugha zinazozungumzwa na wengi pekee.
-